

## **TANGAZO**

Mkuu wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (Eastern Africa Statistical Training Centre) kilichopo Changanyikeni Dar es Salaam, anawatangazia umma na wahitimu wote kuwa Mahafali ya nane (8) yatafanyika siku ya Ijumaa tarehe **02 – 12 – 2022** chuoni Changanyikeni Dar es Salaam.

Wahitimu wote wanatakiwa kuthibitisha ushiriki wao katika mahafali hayo kwa kulipia gharama za majoho ambazo ni shilingi **50,000/-** kwa kila mhitimu. Mwisho wa kuthibitisha ushiriki ni tarehe **25-11-2022** Na mwisho wa kuchukua majoho kwa wahitimu ni **Alhamisi** tarehe **01-12-2022**.

Wahitimu wanatakiwa kutengeneza namba za malipo (Control Number) kupitia link ya [payment.eastc.ac.tz](http://payment.eastc.ac.tz) na kuchagua Bill type ya “**General Services Other Services Collections**” na kulipia kwenye akaunti za chuo za **CRDB** au **NBC** na kisha kutuma risiti za malipo kwa barua pepe ya [admission.officer@eastc.ac.tz](mailto:admission.officer@eastc.ac.tz)

Wahitimu wote wanakumbushwa kuhudhuria mazoezi (rehearsal) chuoni Changanyikeni - Dar es Salaam tarehe **02-12-2022** saa tatu na nusu asubuhi.

Pia, Mkuu wa chuo anawaalika wahitimu wote katika kongamano la tano (5) la kitaaluma la Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika litakalofanyika Alhamisi tarehe **01 – 12 – 2022** chuoni Changanyikeni Dar es Salaam.

Upatapo taarifa hii, mtaarifu na mwenzako.

**WOTE MNAKARIBISHWA**